# “Upendo wa Mwenyezi Mungu kwa Waislamu” 2

## Kwa Nini Mwenyezi Mungu aliwakataa Israeli wa Kale!

BISMILA-HIR RAHMA-NIR RAHIM

بسم الله الرحمن الرحيم

Assalamu’ Aleikum!

Kuna swali moja ambalo Waislamu wote wenye mawazo mapana wanapaswa kujiuliza. Israeli wa Kale, yaani, Wayahudi, wakati fulani walikuwa wateule wa Mwenyezi Mungu. Kwa nini, basi, walikataliwa baadaye?

Sura 5:44 “Hakika tuliteremsha (kwa Musa) Taurati yenye uongozi na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia (walihukumu kwa hiyo Taurati), kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu (hicho) cha Mwenyezi Mungu; nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi (ninyi Waislamu) msiwaogope watu, bali niogopeni (mimi). Wala msibadilishe Aya zangu kwa thamani chache (ya duniani). Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.” 005.044 Al-Maidah

### *Masihi Isa alitabiriwa…*

Kwa nini walikataliwa wasiwe wateule wa Mwenyezi Mungu? Ni dhahiri kwamba Mwenyezi Mungu hakupenda Wayahudi wakataliwe, wala kwamba wao wamkatae Masihi Isa!

Masihi Isa angekuwa nabii kama Musa. Katika Kumbukumbu la Torati 18:15 Musa aliandika… “BWANA, Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye.”

Unabii huu ulitimizwa katika maisha ya Masihi Isa. Injili Matendo 3:20-22 inasema hivi kumhusu Isa… “(Mwenyezi Mungu) apate kumtuma Kristo Yesu, … Kwa maana Musa kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi.”

Kwamba Masihi Isa angezaliwa na bikira ilitabiriwa pia kwa wazi na nabii Isaya. Taurati Isaya 7:14 “Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli.”

Unabii huu ulitimizwa - Injili Mathayo 1:18,21 “Mariamu … alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu [Ruh wa Mwenyezi Mungu].”

Hata mahali halisi kilipokuwapo kijiji alimokuwa azaliwe Masihi Isa kilitabiriwa waziwazi. Taurati, Mika 5:2 “Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele…”

Twaona kutimia kabisa kwa unabii huu wa zamani… Injili, Mathayo 2:1 “Yesu (Isa) alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi.”

Katika Zaburi 72:10 imeandikwa… “Wafalme wa Tarshishi na visiwa na walete kodi; Wafalme wa Sheba na Seba na watoe vipawa.” Twaona kwamba hayo yalitimia katika Mathayo 2:2,11. “Mamajusi (Wenye Hekima) walitoka Mashariki kuja Yerusalemu kumwabudu, walimpa zawadi: dhahabu na uvumba na manemane.”

Kuhusu kazi yake ambayo Masihi Isa angeweza kuifanya ilitabiriwa pia waziwazi. Taurati, Isaya 35:5,6 “Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa. Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba…”

Unabii huu ulitimizwa. Injili Mathayo 11:4-6 “Yesu (Isa) akajibu akawaambia, Nendeni mkamweleze Yohana (Yahya) mnayoyasikia na kuyaona; vipofu wanapata kuona, viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema.”

Isa angekataliwa na Wayahudi. Zaburi 118:22 “Jiwe walilolikataa waashi limekuwa jiwe kuu la pembeni.”

Injili Mathayo 21:42. “Yesu akawaambia, Hamkupata kusoma katika Maandiko, Jiwe walilolikataa waashi, hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni; Neno hili limetoka kwa Bwana, nalo ni ajabu machoni petu.”

Yule aliyekuwa karibu sana miongoni mwa wanafunzi wake Isa angemsaliti. Zaburi 41:9 “Msiri wangu tena niliyemtumaini, aliyekula chakula changu, ameniinulia kisigino chake.” Hilo lilitimizwa: Injili Yohana 13:18-21. “Sisemi habari za ninyi nyote; nawajua wale niliowachagua; lakini andiko lipate kutimizwa, Aliyekula chakula changu ameniinulia kisigino chake.…Amin, amin, nawaambieni, mmoja wenu atanisaliti [maneno haya yanamhusu Yuda Iskariote ambaye usiku ule ule alimsaliti Isa kwa makuhani wa Kiyahudi.]”

Maadui zake Isa wangemtendea jeuri. Taurati Isaya 50:6 “Naliwatolewa wapigao mgongo wangu, na wang’oao ndevu mashavu yangu; sikuficha uso wangu usipate fedheha na kutemewa mate.” Hayo yalitimia: Injili Marko 14:65 “Wengine wakaanza kumtemea mate, wakamfunika uso, na kumpiga makonde.” Injili Yohana 19:1 “Basi ndipo Pilato alipomtwaa Yesu, akampiga mijeledi.” [Akaruhusu apigwe mijeledi]

Isa angepigwa, kisha wafuasi wake wangetawanyika. Taurati Zekaria 13:7 “Mpige mchungaji, nao kondoo watatawanyika.”

Hilo lilitimizwa. Injili, Mathayo 26:56 “Ndipo wanafunzi wote wakamwacha, wakakimbia.”

Nabii Zekaria alitabiri juu ya kiasi cha fedha ambacho Wayahudi wangemlipa Yuda kwa kumsaliti kwao. Taurati Zekaria 11:12 “Mkiona vema, nipeni ujira wangu; kama sivyo, msinipe. Basi wakanipimia vipande thelathini vya fedha, kuwa ndio ujira wangu.” Hayo yalitimia. Injili Mathayo 26:15 “Wakampimia [Yuda] vipande thelathini vya fedha.” Pia Mathayo 27:3-5 “Kisha Yuda … akawarudishia wakuu wa makuhani na wazee vile vipande thelathini vya fedha, akasema, Nalikosa nilipoisaliti damu isiyo na hatia. … Akavitupa vile vipande vya fedha katika hekalu…”

Yatupasa kutambua kuwa Isa hakuja kama Wayahudi walivyotarajia aje. Wao walitaka mtawala ambaye angewafukuzilia mbali Waroma kutoka katika nchi yao. Isa

aliposhindwa kufanya vile walikataa kumtambua. Isa alitumwa akiwa na utume tofauti na ule. Alipaswa kuwa kafara (dhabihu) kwa ajili ya dhambi za wanadamu wote. Taurati Isaya 53:4-6 "Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu … Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu. … Na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote." Hayo yalitimia. Injili Mathayo 20:28 "Mwana wa Adamu [alikuja] kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi."

Lakini Wayahudi waliyakataa hayo yote, na hatimaye Isa aliwaambia… "Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa." Injili Mathayo 23:38 Mwenyezi Mungu aliliacha Hekalu pamoja na Taifa lile. Katika mwaka wa 69 B.K. Tito, Mroma, akaja na kuuharibu Yerusalemu, na Hekalu lile tukufu na kuwaua zaidi ya milioni moja ya Wayahudi. Fundisho hili la kihistoria ni kwa ajili yetu sisi.

Mpendwa mtumishi wake Mwenyezi Mungu, leo na tuipokee fidia yake kwa ajili ya dhambi zetu. Na tusiwe kama Wayahudi wale wa kale waliomkataa yule aliyeteremshwa. Lakini ni afadhali tupokee Toleo hili la Rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ambaye ni Masihi Isa. Hebu kwa unyenyekevu tutii, na kupokea cho chote kinachoteremshwa kutuokoa sisi milele. Leo hii Mwenyezi Mungu na akupe wewe amani ya milele.

## "Poza la (dawa ya) yale yaliyomo vifuani"

Dunia yetu leo iko ukingoni mwa maangamizi. Kila mahali unakotazama unaona wanadamu wamefikia mahali ambapo uchoyo unatawala. Vita vimepamba moto, migongano iko kila mahali, maovu ya binadamu huonekana katika kila taifa, hakuna walioachwa. Jinsi ya kupata fedha kwa gharama yo yote ni mawazo yaliyo katika mioyo ya mamilioni. Kujipenda binafsi kumekithiri kiasi kwamba ni wachache mno wanaowajali wenzao. Je, hayo yatakoma? Nani anayeijua dawa ya kutibu moyo wa kibinadamu uliojaa ubinafsi? Ni Mwenyezi Mungu peke yake ajuaye. Yeye tu ndiye analo suluhisho la ugonjwa wa dhambi ulio ndani ya moyo wa kibinadamu.

Ni wachache mno jinsi gani wanaotambua kwamba dunia hii inaharakisha kufika mwisho wake na ya kwamba maisha juu ya dunia kama tuyajuavyo yatakoma upesi. Muda wetu wa kupimwa karibu sana utakoma, lakini ni wachache mno wanaofahamu kile Mwenyezi Mungu anachotaka kufanya. Siku ya Kiama itakuja kwetu upesi sana. Sura 2:62 "Katika walioamini (Mitume ya zamani huko) na Mayahudi na Wakristo na Wasabai; ye yote (miongoni mwao) atakayemwamini Mwenyezi Mungu … na akaamini Siku ya Mwisho na akafanya vitendo vizuri, basi watapata thawabu zao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika." Al Baqarah 62

Kuhusu siku zetu…(Taurati) Sefania 1:14 "Hiyo siku ya BWANA iliyo kuu i karibu; i karibu, nayo inafanya haraka sana; Naam, sauti ya siku ya BWANA; Shujaa hulia kwa uchungu mwingi huko!"

Ni mapenzi yake Mwenyezi Mungu ya kwamba moyo wa kibinadamu upate kutakaswa kutokana na ugonjwa uitwao dhambi. Ugonjwa huu umeingia ndani ya kila moyo, lakini ni nani aijuaye tiba yake, nani amemwendea Mwenyezi Mungu ili apate kutakaswa? Nani anafahamu kile Mwenyezi Mungu anachotaka kufanya. Nabii yule wa jangwani aliitaja dhambi zaidi ya mara 60 katika Kurani Tukufu. Lakini, je, mimi naushughulikiaje ugonjwa huu? Liko Tumaini Moja tu…

### *Kumtafuta Tabibu…*

Wengine hawajui maana yake tunaposema dhambi! Dhambi ni kutokuwa na amani na Mbingu. Ni kuzivunja au kuzihalifu Amri Takatifu na za Haki za Mwenyezi Mungu, yaani, zile Amri Kumi. Dhambi huja na adhabu yake…mauti ya milele. Dhambi yaweza kusamehewa…

Al-Ghafir 3 "Anayeghufiria dhambi na anayepokea toba, Mkali wa kuadhibu, Mwenye ukarimu; hakuna aabudiwaye kwa haki ila yeye; (na) marejeo ni kwake." Sura 40.3 [Mungu Asameheye]

Mungu ndiye Tabibu Mkuu ambaye peke yake aweza kuuponya ugonjwa wa dhambi.

Mwenyezi Mungu anao mpango wake na unafaa sana. Mamilioni wametafuta msaada kutoka kwake na kupata nafuu baada ya kupata maumivu na huzuni iletwayo na dhambi. Mwenyezi Mungu ana uweza wote, yeye hanaswi ghafula asijue jinsi ya kulishughulikia tatizo la dhambi ndani ya moyo wa kibinadamu.. Tangu siku zile za wazazi wetu wa mwanzo, Adamu na mkewe Hawa, baada ya kula matunda ya mti ule waliokatazwa wasile wakawa wenye dhambi wa kwanza. Basi wanadamu wamehitaji tiba ambayo ni Mwenyezi Mungu peke yake awezaye kutoa. Katika vizazi vyote, wanaume na wanawake wamemtafuta Mwenyezi Mungu na kupata amani mioyoni mwao pamoja na kupata nafuu katika maisha yao kuhusiana na hilo tatizo la dhambi - kuiba, kusema uongo, kudanganya, chuki, ugomvi, uzinzi, kuua, kusingizia wengine au kuzisujudia sanamu, mawazo machafu, orodha hii inaendelea bila kikomo.

Watu wamejaribu wawezavyo …lakini bado moyo mchafu wa kibinadamu haujapata tiba yo yote mbali na ile ya Mwenyezi Mungu. Ni Yeye peke yake aliye na tiba hiyo. Wewe pia waweza kuipata tiba hiyo. Inaelezwa wazi kwamba kwake yeye kuna msamaha. Al-Ghafir 3. Hatuna haja ya kungoja zaidi

### *Tiba ijulikanayo…*

Angekuwa Tabibu wa aina gani kama Mwenyezi Mungu angetuambia tu ugonjwa tulio nao, lakini asingekuwa na tiba? Yeye ajua yote, tena analo suluhisho kwa ajili yako wewe rafiki mpendwa.

Mpango wake Mwenyezi Mungu ni kusamehe dhambi na kututakasa mbali nayo!

Mpendwa msomaji, je, unayo huzuni kwa jambo fulani ujualo kuwa ulikosa? Kwa Mwenyezi Mungu kuna msamaha. Anapokea kwa furaha toba yako. Toba kwa maana rahisi ni kuwa na huzuni ndani ya moyo kwa ajili ya dhambi, jambo ambalo linamfanya mtu huyo atamani kuacha kuendelea katika dhambi. Sura 7:153

"Na wale waliofanya mabaya, kisha wakatubu baada yake na kuamini, Mola wako, baada ya haya (mazuri waliyofanya sasa, atawasamehe) kwani yeye ndiye Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu." Al-Aaraf 153

Yatupasa kumwendea Mwenyezi Mungu kwa dua, na kuungama kwamba sisi tumetenda dhambi, na kwa moyo wenye huzuni tunatubia tendo tulilofanya katika mioyo yetu. Tunapewa ahadi kwamba Mwenyezi Mungu atasamehe. Nani abebaye adhabu kwa ajili ya dhambi zetu? Sikuzote ni lazima mtu fulani alazimike kulipa!

Dhambi daima ina gharama yake, siku zote mtu fulani ni lazima alipe. Dhambi daima ina gharama yake na gharama hiyo ni kubwa.

Ili Mwenyezi Mungu aweze

kusamehe dhambi, analazimika kulipa gharama kwa ajili ya dhambi zetu. Gharama ya dhambi ni kubwa sana…ni mauti, mauti ya milele!

Injili Warumi 6:23 "Kwa maana mshahara wa [gharama ya] dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu!"

Ilikuwa ni kwa njia ya Masihi Isa kwamba Mwenyezi Mungu aliweza kusamehe dhambi. Yeye alikuwa ndiye Mchukuzi Mkuu wa Dhambi zetu! Basi ni kwa njia ya Isa, Mwenyezi Mungu ataiandika sheria yake ya upendo katika mioyo yetu ya kibinadamu. Ni juu yetu kumpokea Isa kama Mwokozi wetu binafsi aliyetuokoa kutoka dhambini na kutoka katika matokeo yake, yaani, mauti! Kumbuka kwamba mtu fulani ni lazima alipe kwa ajili ya dhambi yako. Haki yake Mwenyezi Mungu haiwezi kuacha kutilia maanani uhalifu wa dhambi kama vile Hakimu wa mahakama za kidunia asivyoweza kupuzia uhalifu uliotendwa hapa. Haki inadai adhabu. Isa alilipa adhabu, yaani, ile adhabu kwa ulimwengu mzima, lakini ni wachache mno jinsi gani wanaokubali kulipiwa malipo hayo kwa ajili ya dhambi zao. Leo hii mpendwa msomaji Isa anakukaribisha umpokee na kupokea malipo yake kwa ajili ya dhambi yako.

*Ni mwujiza tu…*

**Sheria ya Mwenyezi Mungu huandikwa katika moyo wa kibinadamu**

Kile kilichoandikwa kwa kidole cha Mwenyezi Mungu juu ya mbao za mawe, hakina budi kuandikwa juu ya mioyo ya nyama kiasi kwamba sisi sasa tutataka kumtii Mwenyezi Mungu. Hivyo swali liko mbele ya kila mmoja wetu, je, nitamruhusu Mwenyezi Mungu kuugeuza moyo wangu, yaani, mawazo yangu yapate kumtii yeye na Sheria yake? Ni kwa njia ya Masihi Isa mwujiza huo unatokea. Tunapomruhusu kufanya mwujiza huo, ndipo anatupatia sisi amani na furaha ya mbinguni.

Ni kitu gani, mpendwa msomaji, kinachokuzuia wewe usimkiri Isa wa Kurani na wa vile Vitabu Vitakatifu ili aichukue dhambi yako na kulipa deni lako. Ni wewe tu uwezaye kuchagua. Mwombe yeye leo katika dua yako faraghani. Ni ombi letu kwamba upate kuionja Amani yake ya milele.

## "Mwenyezi Mungu… Mtakatifu" Al-Hashr 23

"Isa…Mwana Mtakatifu" Maryam 19

Je, hivi yuko mmoja miongoni mwa jamii ya kibinadamu aitwaye Mtakatifu?

Asalamu Aleikum! Amani tamu ya Mbinguni na iwe juu yako. Na ubarikiwe kuwa miongoni mwa wale waliovikwa mavazi ya kijani ya hariri (Al-Khaf 31) na kuegemea matakia ya kijani kibichi (Ar-Rahman 76) katika maisha yale ya baadaye. Mbaraka wa Mwenyezi Mungu Mwenye Rehema Nyingi Sana na Mwenye Huruma sana na uwe juu yako leo hii!

Masihi Isa, ndiye zawadi ya mwana aliye na haki … kwa nini Mwenyezi Mungu, Mtakatifu, atoe zawadi ya mwana aliye mwenye haki au mtakatifu? Kurani Tukufu imemtaja Masihi Isa katika sura zipatazo 15 za Kurani. Hilo bila shaka humaanisha jambo fulani la pekee sana kumhusu Yeye! Anatajwa katika zaidi ya aya 90! Je, huyo alikuwa ni nani? Kusudi lake lilikuwa ni lipi katika kutumwa kwake? Kwa majibu ya maswali haya hatuna budi kumtafuta Mwenyezi Mungu katika sala ya faragha, yaani, dua.

Mwenyezi Mungu alimteremsha Neno kwa wanadamu … Nabii Daudi anatuambia … Zaburi 107:20 "Hulituma Neno lake, huwaponya, huwatoa katika maangamizo yao."

Ni dhahiri kabisa kutoka katika Kurani Tukufu ya kwamba Isa anaitwa "Mtakatifu." Hatuna budi kujiuliza maswali fulani, ni nani aliyemteremsha Isa? Mwanzo alikuwa wapi? Je, alizaliwa na baba wa kidunia? Je, mwanzo wake ulitokana na wanadamu? Hapana, ni wazi kabisa kutoka kwa nabii yule wa jangwani maneno yanasema Isa alizaliwa na mwanamke ambaye hakumjua mwanamume ye yote. Hivyo ni dhahiri kabisa, kwamba Isa alitoka kwa Mwenyezi Mungu. Mtu ye yote anajua fika kuwa huwezi kupata mtoto bila kuwapo mwenzi wa kiume. Lakini hapa yupo mmoja aliyetokea bila kuwapo uhusiano wa mwanamume na mwanamke. Isa anaitwa Mtakatifu, na kwa ajili hiyo ni wazi kabisa kwamba Isa alitoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa maana yawezekanaje kwa mtu awaye yote kutokea kwa mwanamke [peke yake]? Hili humfanya Yeye kuwa Mwana wa Mwenyezi Mungu, si kwa maana ile ya tendo la ndoa, bali kutokana na ukweli kwamba Isa alitoka Mbinguni, kwa sababu Kurani Tukufu yasema wazi kwamba alizaliwa kwa njia ya Roho (Ruh) wa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, Isa alikuwa na silika ya Mwenyezi Mungu kwa kuwa naye alikuwa Mtakatifu. Ni nani miongoni mwa wana wa wanadamu aliyepata kuzaliwa akiwa mtakatifu? Injili Warumi 3:10 "Kama ilivyoandikwa, ya kwamba, Hakuna mwenye haki hata mmoja."

Walakini, wasomi wengi leo wanajitahidi sana kukana kwamba Isa hakuteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kama Mwana wake Mwenyezi Mungu. Kwa nini hilo liwe gumu sana kwetu kulielewa? Upendo wa Mwenyezi Mungu alio nao kwa dunia hii, ulimfanya aje hapa kujifunua mwenyewe kwetu kwa njia ya utukufu sana, njia ambayo kamwe haijawahi kufunuliwa. Tuna udhihirisho mkuu huu wa Mwenyezi Mungu uliofunuliwa kwetu kwa njia ya Masihi Isa. Jina lake na lihimidiwe milele. Haijapata kutokea kamwe huko nyuma katika historia ya kibinadamu wanadamu kumwona Mwenyezi Mungu alivyo hasa. Isa aliweza kuondoa huko kutomwelewa vizuri Mwenyezi Mungu. Basi, Isa alipokuja kwa njia ambayo ilikuwa tofauti na maoni ya Wayahudi yaliyopotoka walimkataa katakata na jambo hilo hatimaye lilisababisha mji wao mtakatifu kuangamizwa na Waroma mwaka 70 B.K. Endapo sisi twaweza kumkataa Isa, ajali yetu bila shaka itakuwa ni ile ile.

Isa anaitwa Mtakatifu, hakuna mtu mwingine ye yote katika Kurani Tukufu aitwaye Mtakatifu, wala hata yule nabii wa jangwani. Hilo linamfanya Isa kuwa mtu wa pekee kweli kweli.

Neno lilo hilo "Mtakatifu" linatumiwa na nabii wa zamani Isaya. Zingatia yale aliyoyaandika juu ya Isa.

Taurati Isaya 49:7 "BWANA, mkombozi wa Israeli, Mtakatifu wake, amwambia hivi yeye anayedharauliwa na wanadamu; yeye anayechukiwa na taifa hili; yeye aliye mtumishi wao watawalao; Wafalme wataona, watasimama; Wakuu nao watasujudu; kwa sababu ya BWANA aliye mwaminifu, Mtakatifu wa Israeli aliyekuchagua." Daudi, Zaburi 72:10,11.

Je, si jambo la ajabu kwamba mtu huyu mkuu ambaye Mwenyezi Mungu angemtuma, angedharauliwa na kuchukiwa na sehemu kubwa ya wanadamu?

Masihi Isa ni muujiza kweli utokao mbinguni. Isa hakuwa na baba yake wa kidunia. Katika Maryam 20 ananukuliwa Mariamu akisema "… hajani-

gusa mwanamume (ye yote kwa njia ya halali)…" Sura 19:20

Roho (Ruh) wa Mwenyezi Mungu alikuwa amemfunika Mariamu, naye akapata mimba. Huko ni kuzaliwa kwa ajabu kabisa.

Nabii yule wa zamani Isaya alitabiri juu ya kuzaliwa huko kwa muujiza muda mrefu kabla hakujatokea. Taurati, Isaya 7:14. "Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli." Neno hili 'Imanueli' maana yake halisi ni 'Mungu pamoja nasi'!

Isaya anaendelea kutabiri juu ya kazi maalumu atakayofanya Isa … Isaya 35:5-6 "ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa. Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba…" Yote hayo yalitimizwa katika maisha yake Masihi Isa! Injili Mathayo 11:5 "vipofu wanapata kuona, viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema."

Isa hakuja kwa njia ile waliyotarajia aje! Hakuja kwa fahari, wala kwa itifaki, tena alizaliwa katika zizi la ng'ombe kule Bethlehemu, wakuu wa ulimwengu wa kipindi kile wakiwa hawana habari, lakini wanyonge waliokuwa wakijifunza (habari zake) wakamsujudia na kumtambua kuwa ni zawadi ya pekee kwa wanadamu iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu. Malaika wa mbinguni walishuhudia tukio lile na kushangilia kwa furaha kuzaliwa kwake. Injili Luka 2:12-14 "Na hii ndiyo ishara kwenu, mtamkuta mtoto mchanga [Isa] amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe. Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema, 'Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia.'"

Isa alikuja si kama Wayahudi walivyotarajia kuwa atasimamisha ufalme wake duniani, lakini Isa alikuja kuanzisha ufalme wa kiroho. Injili Yohana 18:36 Isa alimwambia waziwazi Pilato, mtawala wa Kiroma… "Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa." Si kwa upanga ufalme wa Mungu unaanzishwa bali ni kwa ile kweli na kwa upendo unaojitoa mhanga. Injili Mathayo 26:52 "Ndipo Yesu akamwambia, Rudisha upanga wako mahali pake; maana wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga. "

Si kwa upanga ufalme wa Mungu unaenezwa, bali kwa upole na upendo unaojikana nafsi kwa ajili ya watu. Cho chote chini ya hapo ni udanganyifu. Kwa maana sharti moyo ushawishike na kukubali, na moyo haushawishiki kamwe kwa kutumia upanga. Upanga ni tendo la nje ambao kama ukitumika utaleta tu kulipiza kisasi na chuki nyingi, lakini njia za Mwenyezi Mungu ndizo tu ziletazo mafanikio.

Isa, alitumia muda wake mwingi pamoja na watu duni na wale ambao Wayahudi walidhani ni watu waliotengwa na jamii, wale ambao Wayahudi waliwadharau na kuwaona kuwa hawafai kuokolewa. Injili Marko 2:15-17. "Hata [Isa] alipokuwa ameketi chakulani nyumbani mwake, watoza ushuru wengi na wenye dhambi waliketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake; kwa maana walikuwa wengi wakimfuata. Na waandishi na Mafarisayo walipomwona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi, waliwaambia wanafunzi wake, Mbona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi? Yesu aliposikia aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."

Mpendwa rafiki leo Isa yuko mbinguni kama Kuhani wetu Mkuu, yuko mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, akihudumu kwa ajili yetu. Alibeba dhambi zetu juu yake Mwenyewe na kutoa maisha yake kuwa fidia kwa wengi. Leo Mtakatifu Huyo anasema nawe, yeye ndiye mfereji unaotufungulia njia inayotuunganisha na Mbingu. Hakuna kiwango cho chote cha matendo mema kinachoweza kutupatia sisi sifa kule Mbinguni, ni lazima iwe kwa Neema au wema wa Mwenyezi Mungu peke yake. Vinginevyo, tungekuwa na kitu fulani cha kujisifia kule mbinguni tukisema kwamba tulifika kule kwa matendo yetu mema na hekima yetu wenyewe. Kumbuka Neema ni Neema tu ikiwa ni zawadi. Neema ni upendeleo wake Mwenyezi Mungu bila ya sisi kuongeza kitu cho chote juu yake. Mwenyezi Mungu kwa rehema yake na azidi kutuongoza tunapotafuta kufanya mapenzi yake..

## 'Kamba ya Matumaini'

Je, ni nani huyu ambaye ni Kamba ya Matumaini?

### *"Mtu Aanguka kutoka Melini"*

Sisi sote tumewahi kusikia visa vya wale waliokwenda baharini wakipanda vyombo vikubwa au vidogo. Kama itukiavyo mara kwa mara kitu fulani husababisha mtu fulani kuanguka majini kutoka katika chombo, labda hutokana na kule kugeuka ghafula kwa meli au dhoruba kali ambayo humfanya mtu asiyejihadhari atupwe katika vilindi vya mawimbi. Ndipo kilio kikali husikika hewani … "mtu ameanguka kutoka melini". Kwa haraka wote walio kwenye staha ya meli wanajitahidi sana kadiri wawezavyo kumwokoa mtu yule mwenye bahati mbaya. Kamba zinaletwa na kwa kawaida kifaa fulani hufungwa mwisho wa kamba anayotupiwa mtu yule mwenye bahati mbaya aliye kule kwenye mawimbi. Kama mtu yule anaweza kuogelea kamba hiyo inaweza kusaidia, lakini wakati fulani mtu fulani mwingine anajitoa mhanga na kujitosa baharini kusaidia kumwokoa mtu yule. Kamba ile inatupwa kwa mtu yule, kisha mtu yule huvutwa hadi kwenye usalama chomboni tena.

Kwa njia inayofanana sana na hiyo dunia imepotea mbali na uumbaji mkubwa mno wa Mwenyezi Mungu. Adamu na Hawa walinaswa katika bustani ile ya raha isiyo na kifani walipokuwa hawajihadhari. Kwa njia ya anguko lao, dunia hii imeanguka kutoka katika chombo kwa udanganyifu wa Shetani. Ni kwa uchaguzi wetu wenyewe tumefanya hivyo, na sasa tunaogelea katika matope ya uovu wa dunia hii na tuko katikati ya mawimbi ya giza tukijitahidi kwa nguvu zetu zote kukabiliana na maonjo na matatizo, majaribu na shida za maisha haya zinazotuzunguka pande zote. Twende kwa nani ili tupate msaada kabla hatujazama na kufa. Je, hivi matumaini yako kwa kila mmoja wetu?

Kurani Tukufu yatuambia sisi kwa njia ya pekee sana:

"Na shikamaneni kwa kamba (dini) ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu. (Zamani) mlikuwa maadui; naye akaziunganisha nyoyo zenu; hivyo, kwa neema yake, mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto (wa Jahannam), naye akakuokoeni nalo.

Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake ili mpate kuongoka."

Aali Imran 103 [Sura 3:103]

Leo sisi twaweza kuwa na shukrani kwa ajili ya Neema ya Mwenyezi Mungu, kwa Neema yake hiyo anatuokoa!

Mwenyezi Mungu Muumbaji wetu anatutupia sisi "kamba ya matumaini". Sisi tulikuwa maadui, lakini kwa neema yake twaweza kuwa ndugu. Ni lugha iliyoje hiyo inayofahamika na kututia moyo ambayo twaisoma katika Injili iliyoteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

### *Mwenyezi Mungu atoa zawadi …*

"(Malaika) akasema: 'Hakika Mimi ni mjumbe wa Mola wako: ili nikupe mwana mtakatifu."

Maryam (19): 19

"Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima." Injili Warumi 5:10. "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu." Injili Waefeso 2:8. "Mungu alikuwa akiirejesha dunia kwake kwa njia ya Kristo [Masihi Isa]. Hakuwahesabia watu dhambi zao. Mungu ametupa sisi amana ya ujumbe wake ili watu wapate kurejeshwa kwake."

2 Kor. 5:19 New International readers version

Huyo ni nani ambaye ni Kamba ya Matumaini? Masihi Isa ndiye ile kamba iliyotupwa kwetu. Huyo si kitu kingine bali zawadi (kipawa) kutoka mbinguni kwa ajili ya dunia hii. Hebu kwa shukrani na tuishikilie sana "Kamba" hii."

Ingawa yeye alikuwa umoja na Mwenyezi Mungu (Yohana 10:30) na ndiye yule "Neno" atokaye kwa Mwenyezi Mungu (Aali Imran 39,45), hata hivyo yeye alionja mateso makali sana tunayoyapitia. Aliona nguvu ya majaribu ambayo sisi tunaijua fika. Akawa chombo kilichoteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu na mbingu yote ili kuturejesha tena kwenye usalama. Katika makao yetu ya mwanzo kule Edeni, wazazi wetu wale wa kwanza walipotea, na sisi sote tumefuata nyayo zao. Mtu fulani ilibidi aturudishe kwenye usalama. Hivyo Isa alikuwa ndiye Yule Mmoja aliyejitupa katika dunia hii ya dhambi na aibu na katika vilindi vya mawimbi amekuja kutuokoa.

### *Ngazi toka Duniani hadi Mbinguni!*

Isa aweza kulinganishwa na ngazi. Kama tunataka kufika mbinguni, [ngazi] iko mbali juu yetu. Juu kupita uwezo wetu wa kibinadamu wa kuifikia, sharti tuwe na ngazi. Ngazi hiyo ni lazima ifike mbinguni.

Inapokuja juu ya kuokolewa kwetu kutoka katika dunia hii, msaada wote utokao Mbinguni ungekuwa mfupi mno kutufikia bila ya kuongezea urefu wa mtu mmoja: mtu huyo ni Masihi Isa. Katika Injili anajulikana kama Mwana wa Adamu. Luka 19:10 "Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kilichopotea." Mathayo 20:28 "Kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi."

Mathayo 24:37-39 "Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu."

Masihi Isa arudipo, anakuja kama Mwana wa Adamu. Ufunuo 14:14 "Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi mmoja, mfano wa Mwanadamu, mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa chake, na katika mkono wake mundu mkali."

Vivyo hivyo, sala zetu, dua zetu, kazi zetu nzuri za kutoa sadaka, matendo yetu mema, huenda hayo yakaonesha nia yetu njema, lakini hayatoshi kutufikisha mbinguni pasipo kuongezewa urefu wa mtu mmoja … na mtu huyo ni Kristo Yesu, Masihi Isa. Yeye ndiye kiunganisho chetu kinachotuunganisha sisi na Mbingu ambaye aliteremshwa kwa ajili yetu sisi. Vitabu Vitakatifu hunena hivi… "Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu." Injili Wakolosai 1:27

### *Masihi Isa na Utakatifu wake…*

Alikuwa na kitu gani kilichomfanya awe wa pekee sana? Kurani Tukufu yasema kwamba alikuwa na Roho Mtakatifu…

"Tulimpa Musa Kitabu na tukawafuatisha Mitume (wengine) baada yake, na tukampa Isa, mwana wa Mariamu, hoja zilizo waziwazi, na tukamtia nguvu kwa Roho Mtakatifu …" Al Baqarah (2):87

"Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu [Ruh wa Mwenyezi Mungu] akishuka kama hua, akija juu yake."… Injili Mathayo 3:16.

Isa alikuwa na Ruh (Roho) wa Mwenyezi Mungu. Siyo tu kwamba alikuwa mwanadamu, aliyezaliwa na mwanamke, bali Yeye alikuwa Mtakatifu, na Mwenye Haki. Wanadamu wote waliozaliwa na mwanamke, walizaliwa katika uovu. Tangu anguko la Adamu, watu wote waliozaliwa, wamezaliwa wakiwa na asili iliyoanguka. Kwa maneno mengine, wamezaliwa wakiwa wametengwa mbali na Mwenyezi Mungu. Haikuwa hivyo kwa Masihi Isa, yeye alizaliwa kwa uweza utokao Mbinguni. Ni mtu wa pekee sana, Mtakatifu na Mwenye Haki. Zaidi sana yeye ndiye ile kamba yenye matumaini, katika dunia hii iliyoanguka. Watu wote wanaotaka, wanaweza kuokolewa kutoka katika maovu.

Mpendwa rafiki, je, utamruhusu Mwenyezi Mungu kupitia Masihi Isa akutupie hiyo kamba yake? Je, utaishikilia kwa furaha kamba hiyo itokayo Mbinguni?

Sisi pia twaweza kusema, Bwana tuokoe twaangamia … naye ataisikia sauti hiyo na kuturehemu kwa kumtuma Isa kwetu.

"Na shikamaneni kwa kamba (dini) ya Mwenyezi Mungu nyote…" Aali Imran 103

## "Moto Unaowaka"

Mwenyezi Mungu, kwa Neema yake nyingi, akuongoze uukwepe ule "Moto Unaowaka" ambao umewekwa kwa ajili ya wale wote wanaokataa kumtii na kujisalimisha kwake. Sisi na tuwe miongoni mwa wale walio "Mutaqeen" (wacha Mungu) na kupokea haki ya Mwenyezi Mungu!

Leo tunataka kuchunguza somo hili la "Moto Unaowaka" au Moto wa Jahannam. Huo ni nini? Kwa ajili ya nani "Moto Unaowaka" uliwekwa? Ni nani astahiliye kuyakwepa mateso hayo makali? Je, moto huo utaendelea kuwaka milele na milele kama watu wasemavyo mara kwa mara?

Mara nyingi yule Nabii Mstahiki katika Kurani Tukufu alielekeza kwenye Maandiko ambayo Mwenyezi Mungu kwa rehema zake aliyateremsha kwa wanadamu kabla. Yeye alituambia sisi kwamba katika Vitabu Vitakatifu, Tau-

rati, Zaburi na Injili 'mwanga' [nuru] umefunuliwa kwetu (Al-Anbiyaa 48), na huo ni 'uongozi kwa watu' (Aali Imran 3) na vitabu hivyo hata viliitwa 'Kitabu cha Mwenyezi Mungu' (Al-Maidah 44). Wengi walio katika Uislamu leo huonekana wana wazo fulani lenye makosa wakidhani ya kwamba Taurati na Injili vimechafuliwa. Lakini yule Nabii wa jangwani Muhammad daima aliendelea kuwaelekeza watu kwenye vyanzo hivyo ili sisi tupate kujifunza na kuutumia 'ujumbe' huo (Al-Anbiyaa 48) kwa wale watendao haki!

Basi lipo swali hili muhimu! Je, hivi Mwenyezi Mungu angeweza kumwongoza nabii yule ambaye alikuwa hajui kusoma wala kuandika kwenda kwenye vyanzo vilivyochafuliwa? La, hasha, Mwenyezi Mungu ajua lile alitendalo na sisi twatakiwa kuzingatia kile alichoteremsha kwa Musa, Daudi, Masihi Isa na kwa manabii wengi wa siku zilizopita. Anathubutuje mtu awaye yote kulipuuzia onyo hili takatifu?

Kwa hiyo twaenda kwenye mafunuo hayo matakatifu ya Mwenyezi Mungu kwa somo letu la leo.

Je, ule 'moto unaowaka' uliwekwa kwa ajili ya wanadamu aliowaumba Mwenyezi Mungu? Injili Mathayo 25:41 "Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake."

Kamwe halikuwa kusudi lake Mwenyezi Mungu kuangamiza maisha ya mwanadamu katika mioto ya Jahannam. Mwenyezi Mungu hapendi kabisa kwamba alazimike kumwangamiza mtu ye yote katika mioto ile ya Jahannam. Injili inasema wazi kwamba ule 'moto' uliwekwa kwa ajili ya yule 'Ibilisi na malaika zake.' Kamwe halikuwa kusudi lake Mwenyezi Mungu kumwingiza mwanadamu humo. Hata hivyo, yeye atalishughulikia suala hilo la dhambi lililoanzishwa na Ibilisi (Shetani) na kupokelewa na sehemu kubwa ya wanadamu. Suala hilo la dhambi hatimaye litashughulikiwa na wale wanaong'ang'ania kuendelea na dhambi, na kuishikilia dhambi, wala hawataki msamaha unaotolewa bure na Mwenyezi Mungu kupitia Masihi Isa, hao hatimaye wataangamizwa katika ndimi zile zile za moto uliowekwa kwa ajili ya yule Mwovu na malaika zake. Mwenyezi Mungu ametayarisha njia ya kuukwepa [huo moto] kwa wale wote wanaochagua kuukwepa.

### *Swali la Mwenyezi Mungu kwa Wanadamu leo!*

Taurati Ezekieli 33:11 "Waambie, Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi. Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa…"?

Ni sintofahamu ya kutisha kuhusu tabia ya Mwenyezi Mungu kudhani ya kwamba anafurahi kuwaona wale walioumbwa kwa sura yake wakiteseka katika ndimi zile za moto! Yeye anajitahidi kwa kiwango cho chote kile kumtia moyo mwanadamu ili amtafute yeye na kupata msamaha.

Je, hivi ule moto utakuwa ndiyo 'Makao ya Milele' (Fussilat 28) ya wale wasioamini? Je, moto huo wa milele utaendelea kuwaka 'Milele' na hautakuwa na mwisho wake? Je, lisingekuwa jambo jema kwetu 'kufafanua … Moto wa Jahannam ni nini'? (Al-Muddaththir 27).

### *Miji ya Sodoma na Gomora!*

Tunao mfano mzuri kabisa unaoelezea Moto wa Jahannam ni nini katika kisa cha Lutu (Lud), na mji wa Sodoma. "Kama vile Sodoma na Gomora na miji iliyokuwa kando-kando, waliofuata uasherati kwa jinsi moja na hawa, wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili, imewekwa kuwa dalili, wakiadhibiwa katika moto wa milele." Taurati Yuda 1:7

Hapa tunayo picha dhahiri ya 'moto wa milele' unavyopaswa kuwa. Ni moto ambao hakuna mtu au malaika awezaye kuokoka wala hakuna ye yote awezaye kuzizima hizo ndimi za moto. Moto huo utafanya kazi yake bila kuzuiwa na ye yote. Leo kama utatembelea eneo ilipokuwapo ile miji mizuri ya bondeni, ungeweza kuona wazi ya kuwa miji ile haiwaki moto tena! Moto wa milele umezimika! Moto wa milele hauendelei kuwaka tena. Umefanya kazi yake na kuzimika. Miji ile imetoweka katika miale ile ya moto.

Halijasalia hata kaa moja la moto la kuota mahali hapo. Huo ndio utakuwa Moto wa Milele mwisho wa wakati. Ndipo ghadhabu ya Mwenyezi Mungu itakapomwagwa juu ya wote wasioamini wanaokataa kumpokea na kuikataa Neema yake tele iliyotolewa kwa rehema zake kwa wote. Ndipo juu ya wale wote wanaoikataa Neema ya Mwenyezi Mungu, na juu ya malaika walioanguka [Majini] na Ibilisi mwenyewe [Shetani] aliyeiletea adha dunia hii kwa miaka mingi sana, moto ule utaanguka.

"Wakapanda [waovu wote wa dunia] juu ya upana wa nchi, wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji huo uliopendwa. Moto ukashuka kutoka mbinguni, ukawala." Injili Ufunuo 20:9

Mwenyezi Mungu kwa rehema zake mwishowe ataiangamiza kabisa dhambi yote na kazi yake. Ibilisi, yule Mwovu, hataonekana tena kabisa. Taurati Ezekieli 28:19.

"Wote wakujuao kati ya kabila za watu watakustaajabia; umekuwa kitu cha kutisha, wala hutakuwapo tena hata milele." Ezekieli 28:19

Moto huo kamwe hauwezi kuzimwa mpaka umalize kazi yake kama alivyokusudia Mwenyezi Mungu. Huo ndio moto unaowateketeza waovu wote pamoja na Shetani [Ibilisi yule Mwovu na Majini yote]. Katika sura hiyo ya 28 ya nabii Ezekieli tunasimuliwa kidogo historia ya kule alikotoka Shetani, yule Mwovu. Zamani alikuwa malaika afunikaye au kerubi kama ilivyoelezwa katika Kitabu Kitakatifu cha Taurati, Ezekieli 28:14 hapo kale alisimama karibu na kiti cha enzi cha Mwenyezi Mungu na alikuwa malaika anayeng'aa. Baada ya anguko lake na kutupwa kwake chini kutoka Mbinguni, naye pia akaja kwenye Bustani ya Edeni, Bustani ya Raha isiyo na kifani ambayo Mungu alikuwa amekusudia kwa Adamu na mkewe Hawa. Pale Edeni ndipo alipowajaribu watu wale wawili wa mwanzo ili wafanye dhambi. Inasiklitisha kwamba waliacha kumwangalia Mwenyezi Mungu na kuusadiki uongo wa Ibilisi au Shetani.

Mpendwa rafiki wa Mwenyezi Mungu, njia ya kuokolewa imeandaliwa kwa wazao wote wa Adamu ili kuzikwepa zile 'ndimi za moto' ambao utakuja dunia hii itakapofika mwisho wake. Mwenyezi Mungu hakukusudia kamwe kwamba ye yote miongoni mwa jamii ya kibinadamu ateseke katika kile ambacho Kitabu Kitakatifu kinasema ni "mauti ya pili". Hiyo ilikusudiwa kwa yule Mwovu na malaika zake. Mwenyezi Mungu kwa rehema yake nyingi na upendo kwa familia ya Adamu amemteremsha "Mtu fulani" ili apate adhabu tuliyostahili kwa kutenda dhambi. Huyo "Mtu fulani" ni Masihi Isa. Alikuwa Masihi siyo tu kwa Wayahudi waliompokea, bali kwa wote watokao katika familia ya Adamu, ye

yote yule atakayekubali toleo hilo la rehema kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mwenyezi Mungu!

"…Na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure." Ufunuo 22:17. Maji hayo ya uzima ni huyo Masihi Isa ambaye ndiye Mwokozi wa wanadamu! Hata sasa kama Ruh [Roho] wa Mwenyezi Mungu anagusa moyo wako na akili yako, basi, mpokee yeye aliyeteremshwa na Mbingu. Usimsikitishe Mwenyezi Mungu, aliyetoa kwetu kitu hicho cha thamani! Lakini kwa shukrani pokea Rehema yake Mwenyezi Mungu.

### *Nuhu na Gharika ya Maji*

Miaka mingi iliyopita, makusudi mabaya ya wanadamu yalimfanya Mwenyezi Mungu kumsisitizia Nuhu kujenga Safina ambayo ndani yake angejiokoa mwenyewe na familia yake na wanyama wote kila mahali, pamoja na ye yote aliyechagua kuokolewa kutoka katika kaburi la maji ambayo yalikuwa yakija juu ya dunia yote. Wakati ule Mwenyezi Mungu alikuwa ameionya dunia ili itubu na kuachana na uovu wake na kuponywa. Walakini walikataa kujisalimisha wenyewe kwa Mwenyezi Mungu na kuachana na uovu wao. Uovu wao ulikuwa umekithiri mno kiasi kwamba hata Taurati yasema … "BWANA akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote." Taurati Mwanzo 6:5.

La kusikitisha ni kwamba yale maji hayakuweza kuosha hali ya dhambi iliyokuwamo mioyoni mwa wale waliokuja baadaye. Wakamwasi tena Mwenyezi Mungu vizazi vilivyokuja baada ya Nuhu.

Hivi sasa sisi nasi tuko katika hatua za mwisho za historia ya dunia hii. Wakati huu ule mwisho umekaribia ambao Mwenyezi Mungu atalishughulikia kabisa suala hili la dhambi kwa mara ya mwisho pamoja na wale wanaochagua kuing'ang'ania dhambi kuliko kumruhusu Mwenyezi Mungu kwa njia ya Masihi Isa aiondolee mbali dhambi.

Moto huo utakuwa na matokeo yatakayodumu milele, hapatakuwa na ufufuo kwa watakaokufa katika moto huo wa mwisho. Kwa sasa mtu akifa, atakuja kuonekana tena duniani katika ufufuo (kiama) wa siku ile ya mwisho. Lakini ule moto unaokuja utawaangamiza hao wala hawataonekana tena kabisa. Yule Mwovu [Ibilisi], Majini [malaika walioanguka] na waovu wote wasiotibika, wataungua na kuwa majivu juu ya dunia hii.

"Nanyi mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu; katika siku ile niifanyayo, asema BWANA wa majeshi." Malaki 4:3 [Kitabu cha mwisho cha Taurati].

Hakitasalia kitu cho chote ila majivu tu … kuanzia na yule aliyekuwa zamani Ibilisi, laghai, na mawakala wake wote. Kamwe ulimwengu huu ulioumbwa na Mwenyezi Mungu hautaweza kusumbuliwa tena na laghai huyo mkuu, yaani,huyo Ibilisi.

Mpendwa rafiki wa Mwenyezi Mungu, leo unapoisikia sauti ya Mwenyezi Mungu mruhusu Masihi Isa ayaongoze maisha yako na kuyaondolea mbali maisha yako ya dhambi.

### *"Hajiri alivyomwona Mwenyezi Mungu kuwa ni Mwenye Neema…"*

Mpendwa msomaji Neema ya Mwenyezi Mungu na iwe juu yako leo…kwa kuwa Yeye ni Bwana wa [Fadhila] Neema nyingi (Al-Hadyd 29). Tunapovifungua Vitabu Vitakatifu tunamwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu kwamba asikie sala (dua) zetu, ili katika fahamu zetu azidi kufungua Neema yake awapayo wanadamu. (An-Naml 73) Na tuwe miongoni mwa wale wanaoshukuru kwa Neema hiyo.

Somo hili la Neema [Fadhila] lapatikana katika Kurani Tukufu yote na katika Taurati na Injili. Katika Kurani Tukufu peke yake somo hili la "Neema" lapatikana mara 74! Je, hili lisingetuambia kitu fulani juu ya Neema ya Mwenyezi Mungu tunayohitaji kujifunza kwa kina. Neema ni nini?

Kamusi inafafanua "Neema" kuwa ni "**upendo unaotolewa bure kwa asiyestahili, tena ni upendeleo wa Mungu**, ni chemchemi na chimbuko la mibaraka yote wanayopokea wanadamu kutoka kwake."

Kwa hiyo, ikiwa Neema ni **upendo unaotolewa bure kwa asiyestahili,** tena ni upendeleo wa Mungu, maana yake ni kwamba hatuwezi kuipata kwa kufanya kazi…. hivyo ni kipawa (zawadi). Kama tungeweza kuipata kwa kufanya kazi, kuinunua, au kuipata kwa jitihada yetu fulani, basi, ingekoma kuwa "Neema". Je, hivi kuna ajabu yo yote kwamba huyo nabii wa jangwani alisema mara nyingi sana juu ya Neema? Mpendwa msomaji mara 74 Neema inanenwa katika Kurani Tukufu. Wenye dhambi wanastahili mauti, lakini Mungu anatoa Neema. Mpendwa msomaji, u mtafutaji wa Neema yake Mwenyezi Mungu … "tafuta Fadhila [Neema] ya Mwenyezi Mungu… (Al-Muzzammil 20) nawe utaipata hakika ni ahadi yake.

Kuna kisa kimoja kutoka siku zile za kale cha mtu fulani aliyeipata Neema yake Mwenyezi Mungu. Kisa hiki kinatoka jangwani.

Muhammad alisema kwamba sisi tulikuwa na haja ya ku"taja katika Kitabu (hiki) Ismaili" (Maryam 54). Lakini ili kupata kisa kamili tunahitaji kwenda kwenye Biblia (Taurati) Mwanzo sura ya 16 kwa sababu hakipatikani katika Kurani Tukufu! Walakini huyo nabii wa jangwani ametuagiza tukijue kisa cha Ishmaeli. Kwa hiyo Waislamu wanaihitaji Biblia, kusema kweli, Kurani Tukufu haileti maana pasipokuwa na ujuzi wa Biblia. Vingi kati ya visa vilivyo katika Kurani havijakamilika bila ya kufunuliwa kisa chote na Biblia.

Humu, katika Taurati, kinasimuliwa kimojawapo cha visa vinavyosisimua juu ya Neema [Fadhila] ya Mwenyezi Mungu iliyotolewa kwa wanadamu katika Taurati. Wakati huu wote kumbuka kwamba Neema ya Mwenyezi Mungu hakuna hata mmoja wetu anayestahili kuipata. Neema ni kipawa na kipawa hakipatikani kwa kukifanyia kazi, wala kukinunua, vinginevyo, basi, ingekoma kuwa neema.

Katika kisa hiki, yule mtu tajiri Ibrahimu na mkewe Sarai (Sara), wote wawili ni wazee, wala hawana watoto. Sara alikuwa amepita umri wa kuzaa watoto. Miaka mingi mapema, Mungu alikuwa amewaahidi kuwapa mwana. Lakini hawakupata mwana, je, hivi Mungu alikuwa amesahau? Je, alikuwa ameshindwa kutimiza ahadi yake ya kumpa mwana Ibrahimu? "Nalo neno la BWANA likamjia likinena, Huyu hatakurithi, bali atakayetoka katika viuno vyako ndiye atakayekurithi. Akamleta nje, akasema, Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu. Akamwambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako. **[Ibrahimu] akamwamini BWANA**, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki." Mwanzo 15:4-6

Muda unaendelea…Ibrahimu na Sara sasa ni wazee sana na b ado hakuna mrithi, hakuna mtoto ambaye wa-

naweza kumwonesha upendo wao na mahaba yao. Hakuna mrithi wa mali aliyokuwa nayo Ibrahimu. Lakini walikuwa wameahidiwa na Mungu kwamba Ibrahimu angepata mwana. Lakini mpaka wakati huu hakuna mtoto waliyepata. Hivyo Sara na Ibrahimu wanafanya mpango ambao kwa huo wanataka kumsaidia Mungu kutimiza ahadi yake ya kuwapa mrithi. Mwanzo 16:1 Je, hivi Mwenyezi Mungu anahitaji asaidiwe kutekeleza mipango yake? Siku moja Sara akapendekeza mpango fulani, ambao kwa huo Ibrahimu angeweza kupata mtoto.

Kisa hicho kinaendelea katika Taurati…

"Basi Sarai mkewe Abramu hakumzalia mwana, naye alikuwa na mjakazi, Mmisri, jina lake **Hajiri.** Sarai akamwambia Abramu, Basi sasa, BWANA amenifunga tumbo nisizae, umwingilie mjakazi wangu, labda nitapata uzao kwa yeye. Abramu akaisikiliza sauti ya Sarai. Sarai mkewe Abramu akamtwaa Hajiri Mmisri mjakazi wake, baada ya kukaa Abramu katika nchi ya Kanaani miaka kumi, akampa Abramu mumewe, awe mkewe. Basi akamwingilia **Hajiri**, naye akapata mimba. Naye alipoona kwamba amepata mimba, bibi yake alikuwa duni machoni pake." Mwanzo 16:1-4

"Sarai akamwambia Abramu, Ubaya ulionipata na uwe juu yako; nimekupa mjakazi wangu kifuani mwako, naye alipoona kwamba amepata mimba, mimi nimekuwa duni machoni pake. BWANA na ahukumu kati ya mimi na wewe. Naye Abramu akamwambia Sarai, Tazama, mjakazi wako yu mkononi mwako, mtendee lililo jema machoni pako. Sarai akamtesa, naye akakimbia kutoka mbele yake. Malaika wa BWANA akam-

# "Upendo wa Mwenyezi Mungu kwa Waislamu" 2

wona kwenye chemchemi ya maji katika jangwa, chemchemi iliyoko katika njia ya kuendea Shuri. Akamwambia, **Hajiri**, wewe mjakazi wa Sarai, unatoka wapi, nawe unakwenda wapi? Akasema, Nakimbia mimi kutoka mbele ya bibi yangu Sarai. Malaika wa BWANA akamwambia, **Rudi kwa bibi yako**, **ukanyenyekee** chini ya mikono yake. Malaika wa BWANA akamwambia, Hakika nitauzidisha uzao wako, wala hautahesabika kwa jinsi utakavyokuwa mwingi. Malaika wa BWANA akamwambia, Tazama! wewe una mimba, utazaa mwana wa kiume, **nawe utamwita jina lake Ishmaeli**, maana BWANA amesikia kilio cha mateso yako. Naye atakuwa kama pundamwitu kati ya watu, mkono wake utakuwa juu ya watu wote na mkono wa watu wote utakuwa juu yake, naye atakaa mbele yao ndugu zake wote. Akaliita jina la BWANA aliyesema naye, Wewe u Mungu uonaye, kwani alisema, Hata hapa nimemwona yeye anionaye? Kwa hiyo kisima kile kiliitwa Beer-lahai-roi. Tazama, kiko kati ya Kadeshi na Beredi. **Hajiri** akamzalia Abramu mwana wa kiume; Abramu akamwita jina lake Ishmaeli, yule mwanawe, ambaye **Hajiri** alimzaa. Naye Abramu alikuwa mtu wa miaka themanini na sita, hapo **Hajiri** alipomzalia Abramu **Ishmaeli**."

Taurati Mwanzo 16:4-16

Hivi ndivyo mwanadamu alivyotafuta suluhisho kwa tatizo la Abramu la kukosa kuwa na watoto. Lakini mpango wake haukuwa mpango wa Mungu. Hata hivyo Mungu hakuwaacha, bado aliendelea kufanya kazi pamoja nao. Mpango wa Mungu ulikuwa kwamba **Sara** mkewe Ibrahimu amzalie mwana na alifanya hivyo mwishowe. Baada ya miaka mingi zaidi kupita, Sara alipata mimba na kumzalia mwana Ibrahimu katika uzee wao. Ahadi za Mungu hazijui kuharakisha wala kuchelewa. Isaka akazaliwa na Sara wakati akiwa mzee sana, hii ni kwa Neema ya Mungu. Sasa kuna ugomvi mkali nyumbani mwa Ibrahimu baina ya wake zake wawili, Sara na Hajiri.

"Mtoto [Isaka] akakua, akaachishwa kunyonya; Ibrahimu akafanya karamu kuu siku ile Isaka alipoachishwa kunyonya. Sara akamwona yule mwana wa Hajiri Mmisri, ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka. Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu, Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka. Na neno hilo lilikuwa baya sana machoni pa Ibrahimu, kwa ajili ya mwanawe. Mungu akamwambia Ibrahimu, Neno hili lisiwe baya machoni pako, kwa ajili ya huyo mwana, na huyo mjakazi wako. Kila akuambialo Sara, sikiza sauti yake, kwa maana katika Isaka uzao wako utaitwa. Naye mwana wa mjakazi nitamfanya kuwa taifa, maana huyo naye ni uzao wako." Ibrahimu akaamka asubuhi na mapema akatwaa mkate na kiriba cha maji, akampa **Hajiri** akimtwika begani pake, na kijana, akamruhusu; naye akatoka, akapotea katika jangwa la Beer-sheba. Yale maji yakaisha katika kiriba, akamlaza kijana chini ya kijiti kimoja. Akaenda akakaa akimkabili, mbali naye kadiri ya mtupo wa mshale; maana alisema, Nisimwone kijana akifa; naye akakaa akimkabili, akapaza sauti yake, akalia."

Mwanzo 21:1-16

Kufikia hapo kila kitu kilikuwa cha kukatisha tamaa kwa macho ya kibinadamu. Hajiri ametoka kwenda katika joto kali la jangwani, chakula kimekwisha, maji yamekwisha, na yule mtoto anakufa. Anamtupa Ishmaeli chini ya kichaka, kisha analia.

Ni hapo inapoonekana kuwa hakuna tumaini ndipo Neema ya Mwenyezi Mungu huonekana.

"Mungu akasikia sauti ya kijana. Malaika wa Mungu akamwita Hajiri kutoka mbinguni, akamwambia, Una nini, Hajiri? Usiogope, maana **Mungu amesikia** sauti ya kijana huko aliko. Ondoka, ukamwinue kijana, ukamshike mkononi mwako, kwa kuwa nitamfanya kuwa taifa kubwa. Mungu akamfumbua macho, naye akaona kisima cha maji; akaenda akakijaza kiriba maji, akamnywesha kijana. **Mungu akawa pamoja na huyo kijana**, [**Neema**] naye akakua, akakaa katika jangwa, akawa mpiga upinde. Akakaa katika jangwa la Parani…"

Taurati Mwanzo 21:17-21

Mpendwa msomaji je unasumbuka? Je, maisha yako yako katika zahama kama yalivyokuwa yale ya Hajiri jangwani? Si kitu wewe uwe nani Mwenyezi Mungu yuko karibu nawe, Neema yake ni nyingi kwa mwenye dhambi mkuu kuliko wote kama tu utarudi kwake kwa moyo wako wote na kuitafuta Neema yake.

Mpendwa msomaji, leo itafute Neema yake, usichelewe. Mwenyezi Mungu yuko karibu nawe na yuko tayari kukisikia kilio cha mwenye dhambi aliye dhaifu kuliko wote, kama alivyokisikia kilio cha Ishmaeli alipokaribia kufa jangwani, naye akaja kumsaidia. Mpendwa msomaji, nakutakia Amani ya Milele na Neema yake Mwenyezi Mungu.

**Kwa maelezo zaidi:**

www.salahallah.com
www.allahshanif.com
www.swahilitruth.com